

102/3

## KISWAHILI

Karatasi 3

Oktoba 2016

Muda: Saa 2½

# ◦ TATHMINI YA PAMOJA YA GATUZI NDOGO YA KANDARA KIDATO CHA TATU

## KISWAHILI

Karatasi 3

Oktoba 2016

Muda: Saa 2½

## MAAGIZO

- a) Jibu maswali **manne** pekee.
- b) Swali la kwanza ni la **lazima**.
- c) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- d) Maswali mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu ya B, C, D na E
- e) Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

## SEHEMU A : USHAIRI

### 1. Swali la lazima

#### Soma shairi lifuatato kisha ujibu maswali

##### SABUNI YA ROHO

Ewe tunu ya mtima, kwa nini wanikimbia ?  
Ndiwe suluhu za zama, waja wakukimbilia,  
Waja wanakutazama, madeni wakalipia,  
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima

Ndiwe mafuta ya roho, walisema wa zamani  
Utanunua majoho, majumba na nyumbani,  
Umezitakasa roho, umekuwa mhisani,  
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima

Matajiri wanakujuja, wema wako wameonja,  
Nguo zao umefua, wakupata kwa ujanja,  
Sura zao ‘mefufua, wanazuru kila njanja,  
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima

Ndiwe mvunja mlima, onana na maskini,  
Watazame mayatima, kwao kumekua duni,  
Wabebe waliokuwa, wainue walio chini,  
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima

Ndiwe mvunja mlima, wapi kupata uwezo,  
Umezua uhasama, waja kupata mizozo,  
Ndiwe chanzo cha zahama, umewatia vikwazo,  
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima

Umevunja usuhuba, familia zazozana,  
Waliokuwa mahabuba, kila mara wagombana,  
Roho zao umekaba, majumbuni wachinjana,  
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima

Nakutafuta kwa hamu, sabuni unirehemu,  
Sinilipue ja bomu, sije kawa marehemu,  
Niondoe jahanamu, ya ufukara wa simu,  
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima

Naondoka wangu moyo, nikuitapo itika,  
Fulusi wacha uchoyo, tatua yalonifika,  
Nichakeshe kibogoyo, nami nipate kuwika,  
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima

##### Maswali

- i) Taja nafsi nenewa. Thibitisha. (alama 2)
- ii) Eleza toni ya nafsi neni. (alama 1)

- iii) Eleza arudhi zozote nne zilizozingatiwa katika utunzi wa shairi hili. (alama 4)
- iv) Mshairi anawasilisha ujumbe gani katika mleo wa ubeti wa sita ? (alama 1)
- v) Ukitoa mfano, eleza mbinu zozote tatu za lugha alizotumia mshairi. (alama 3)
- vi) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (alama 4)
- vii) Kwa kutoa mifano miwili onyesha jinsi mshairi anatumia ruhusa ya mshairi. (alama 2)
- viii) Kwa kurejelea mpangilio wa vina, eleza bahari ambamo shairi hili linaweza kuainishwa. (alama 1)
- ix) Fafanua maana ya :  
 a) ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima. (alama 1)  
 b) jehanamu (alama 1)

**SEHEMU YA B : TAMTHILIA**  
**T.Arege : Mstahiki Meya**  
**Jibu swalii la 2 au 3**

2. "Iwapo umefanya, yapo mengi mabayo hayakunyooka"  
 a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Tambua mbinu moja iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
- c) Fafanua kauli kwamba "yapo mengi ambayo hayakunyooka" (alama 8)
- d) Eleza jinsi baadhi ya wahusika walijaribu kuyanyoosha. (alama 6)
3. Kwa kutoa mifano kumi, eleza vizingiti walivyokumbana navyo wanacheneo wakati wa kupigania mageuzi. (alama 20)

**SEHEMU YA C : RIWAYA**  
**K. Walibora : Kidagaa Kimemwozea**  
**Jibu swalii la 4 au 5**

4. Kufariki kwa kitoto Uhuru ni jazanda inayoashiria hali halisi ya mambo riwayani. Jadili. (alama 20)
5. "... usiniweke pambeni kama tanbihi, mimi na wanawake wenzangu kama wanaume wengine wafanyakayo waandikapo ..."   
 a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Bainisha tamathali ya usemi iliyotumika hapa. (alama 2)
- c) Onyesha jinsi mwanamke amesawiriwa katika riwaya hii. (alama 14)

**SEHEMU YA D : HADITHI FUPI**

**K. Walibora : Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine**

**Jibu swali la 6 au 7**

6. Mwana wa Darubini (K. Mwende Mbai)  
“Uniulie nini na ndoa yetu na wewe inamhusu pia yeye ?”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Eleza sifa zozote nne za msemewa. (alama 8)
- c) Jadili madhila yanayomkumba mwanamke katika hadithi hii. (alama 8)
7. Jadili jinsi mwandishi amefanikisha anwani yake katika hadithi ya “Shaka ya mambo” (alama 20)

**SEHEMU YA E : FASIHI SIMULIZI**

8. a) Eleza fotaufi tatu kati ya methali na vitendawili. (alama 6)
- b) Jadili njia zozote tatu ambazo jamii ya kisasa hutumia ili kudumisha fasihi simulizi. (alama 6)
- c) i) Maigizo ni nini ? (alama 2)  
ii) Eleza mambo matatu anayopaswa kufanya mwigizaji ili kufanikisha uigizaji wake. (alama 6)